# UMENIFILIA MIMI

*- Kwaresma -*

Martin Mutua Munywoki
Apr 7, 2015
edited 2019



# UMENIFILIA MIMI

Na M. M. Munywoki

1. Ulimwengu umekuhukumu, kwa ajili ya dhambi za wanadamu,
Umeteseka umemwaga damu, mikononi mwao watu wadhalimu.
Umefanya lipi kosa, jinsi wanavyokutesa,
Au lipi lilokupasa, kulitenda ukakosa,
Uteseke jinsi hii, mtini mtupu kabisa.
Umenifilia mimi, nipate uzima wa milele!

2. Wafuasio wamekukimbia, ulo nao wanasinziasinzia,
Yule mtume uloaminia, mtunza fedha Yuda kakusalitia.
Uliyemkweza mwamba, ushujaa unayumba,
Sasa Petro akana kwamba, hakujui pale chemba,
Na wewe husemi neno, ki-nywa chako umefumba.
Umenifilia mimi, nipate uzima wa milele!

3. Yule jambazi wamemweka huru, ila wewe mauti  wameamuru,
Pilato ashindwa kukunusuru, mbele ya umati upigao nduru.
Unapewa msalaba, kichwani taji la miiba,
Mijeledi unapobeba, na makofi wakuzaba,
Mwili wote ni vidonda, unapumua haba haba.
Umenifilia mimi, nipate uzima wa milele!

4. Wakudhihaki wakuchekelea, hata mate wakutemea temea,
Lakini nawe unawaombea, husimami hata ukajitetea.
Vazio wamekupora, wanalipigia kura,
Na yule mamao Bikira, machozi yamfumba sura,
Mkuki wanakuchoma, wanyweshwa siki kukukera.
Umenifilia mimi, nipate uzima wa milele!

5. Ulipokuja humu duniani, ni mapendo katutoe utumwani,
Umejitoa ufe pale mtini,  ili mwisho tufike juu Mbinguni.
Ni pendo zaidi gani, kupita hili jamani,
Kuuweka uhai chini, kwa rafiki wa thamani,
Asante kutukomboa milele milele milele.
Umenifilia mimi, nipate uzima wa milele!

TUTAFAKARI MATESO YA YESU PAMOJA NA MAHANGAIKO YETU YA KILA SIKU
KWA AJILI YA MAISHA BORA YA KESHO, YETU NA YA WENZETU